

Maswali

1. Nabii ni nani?
2. Kazi ya Eliya ilikuwa gani?
3. Wakati watu walikataa Mungu alionyesha upendo kwa Mungu vipi?
4. Alikuwa na uoga lakini mbona alitetea Mungu?
5. Tufanye nini wakati watu wanakataa kumuabudu Mungu?
6. Jina la nabii mgeni liliitwa nani?
7. Elisha alifanya nini kuonyesha amekubali kazi mpya?
8. Elisha alifanya nini ili kujiandaa kuwa mtu wa Mungu?
9. Tunatakiwa tufanye nini kujisaidia tuwe na utawa?
10. Nini itafanyika tukichukuwa watu wasio wa utawa kuwa marafiki zetu?

Majibu

1. Nabii ni mjumbe wa Mungu.
2. Eliya alikuwa akiwambia watu ujumbe wa Mungu hata kama ilizungumzia uovu waliofanya.
3. Eliya alionyesha upendo wake kwa mungu kwa kutetea alichiamini na kuambia watu waache kutenda dhambi na wamgeukie Mungu.
4. Eliya alimtetea Mungu kwa sababu alijua ako haki na Mungu angemsaidia kwa hayo.
5. Inatubidi tuambia marafiki zetu juu ya neon la Mungu na kuwahimiza wamwamini Mungu mmoja aliye wa kweli na kwamba wokovu unapatikana kwa mwana wake.
6. Jina la nabii mgeni ni Elisha.
7. Ng'ombe na kongwa ndio ilikuwa njia ya pekee aliyojipatia riziki ya kila siku, lakini aliteketeza kuonyesha hatarudi kwa maisha ya kale.
8. Elisha alikaa na Eliya kwa mda mwingi ili ajifunze neno la Mungu na awe mtu wa Mungu wa nguvu.
9. Inatulazimu tuwe marafiki na watu wa utawa kwa kukaa nao.
10. Tukiwa marafiki na watu wasio na utawa, tutajifunza mienendo mibaya na pole pole tutamuacha Mungu.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 2



23 Mwito wa Elisha

Marejeo

1 Wafalme 20:19—21

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba kitu cha maana maishani mwetu ni kumtumikia Mungu.

Maneno maalum


1. Eliya + nabii + sanamu + kosa + ogopa + muue + tetea Mungu.
2. Mjumbe + sema ujumbe wa Mungu + hadharisha + maisha mabaya + watu wakakasirika.
3. Sisi + mafunzo ya Mungu + watu hawatutaki.
4. Eliya ana uzuri + Mungu anasaidia + Elisha + lima na ng'ombe + vazi.
5. Kwaheri + moto + piga ng'ombe + usirudi nyuma + maisha mapya.
6. Chukua mda + soma kuwa na utawa + marafiki wabaya + tunakuwa wabaya + kuwa rafiki wa mtu wa utawa.

23.1 Nabii Eliya alikuwa mtu wa ajabu. Watu wengine wote walipoanza kuabudu sanamu na kuacha Mungu, aliwaambia kwamba ilikuwa makosa na lazima waache kutendea Mungu dhambi. Ingawaje aliogopa kwamba atauwawa, ilimlazimu asimame na imani yake kama mtu wa Mungu. Hakutaka watu waendeleo kumkasirisha Mungu.

23.2 Kazi ya Eliya ilikuwa kuambia watu mambo alioambiwa na Mungu. Alikuwa kama mjumbe. Mungu alimpa ujumbe wa watu naye aliwambia huo ujumbe. Ilikuwa kazi ngumu kwa sababu kila ujumbe ulikuwa wa kuwahadharisha kwamba walikuwa wanaishi maisha mabaya. Hakuna anayekubali kuambiwa kwamba anamakosa, kwa hivyo watu wengi walimkasirikia Eliya.

23.3 Haya yanaweza kufanyika kwetu tunapoambia watu chenye Mungu amesema kwa Biblia, wanafikiria ni sisi tumesema lakini ukweli ni Mungu amesema. Huwa tunawambia kwamba hawakai vile wanapaswa kulingana na Biblia.

23.4 Siku moja Eliya alikuwa ameudhika na kazi yake, Mungu akamwambia kwamba alikuwa amepata mtu wa kufanya kazi yake. Jina lake ni Elisha. Elisha alikuwa mkulima, siku moja alikuwa shambani na ng'ombe wake akilima. Eliya alikuja penye alikuwa na akatupa vazi lake juu ya mabega ya Elisha. Elisha alijua kwamba ameitwa kuwa nabii kama Eliya.



23.5 Kwa hivyo Elisha aliaga wazazi wake na akawasha kongwa za ng'ombe wake. Alichinja wale ng'ombe wa kulima juu ya huo moto na kufurahi na rafiki zake. Hii ilikuwa ishara aliyoionyesha kwamba hatarudi kuwa mkulima tena ila atakuwa nabii. Mungu atanipa nguvu za kufanya kazi mpya hata kama ni ngumu mno. Kwa hivyo Elisha akaiacha kazi yake ya zamani na kuanza maisha mapya kama mtu wa Mungu.

23.6 Elisha alichukuwa mda na Eliya akiangalia vile aliishi na kuwa na mazungumzo ya utawa. Hii ilimsaidia vile atakaa kama mtu wa Mungu. Vile vile kama sisi, tukikaa na watu wa Mungu itakuwa mfano mzuri tukiiga kwa hiyo tunapaswa tuangalie watu tunaokaa nao. Wakiwa watu wasio na utawa, hata nasi tutakuwa vivyo hivyo. Kwa hivyo ona kwamba marafiki wako wanampenda Mungu. (soma 1Wakorintho 15:33).